

# Misioni yako ni nini?

*2010.global*

Hamasika. Jihusishe

Tarehe 6 Juni 2010 ni siku inayotoa fursa ya pekee kwa Wakristo wote duniani kusherehekea wito wa Mungu kufanya misioni.

Siku hii imetengwa ili kusherehekea yale yote tuliyopokea kutoka kwa Mungu kwa njia mbalimbali za imani. Pia ni nafasi muafaka wa kujitoa kikamilifu, bila kujali sisi ni nani na tunaishi wapi kumshuhudia Kristo nyakati hizi.

Edinburgh 2010
WITNESSING TO CHRIST TODAY





## Palitokea nini mwaka 1910?

Imetimia miaka mia moja tangu mkutano mkuu wa misioni duniani ulipofanyika kule Edinburgh mwezi Juni 1910. Mkutano huo ulikuwa na Wakristo kutoka makanisa mengi duniani waliohudhuria kuweka mikakati ya jinsi ya kufanya misioni ya kanisa la kikristo ulimwenguni pote. Ingawa wale waliohudhuria walikuwa zaidi wanaume weupe, kutoka nchi za magharibi, ilikuwa hafla ya pekee na ya msingi. Washiriki walitambua haja ya kuvunja mipaka ya ukoloni na kuamua kuyakaribisha makanisa machanga ambayo yalikuwa yanakua yakijitegemea na kujiendesha yenyewe ulimwenguni.

## Nini kilijitokeza?

Tangu wakati huo, Wakristo walijifunza zaidi jinsi ya kufanya kazi pamoja, kumegeana habari njema ya upendo wa Mungu na kumshuhudia Kristo kwa namna mbali mbali hasa kutetea maskini, kupigania haki, kupinga ubaguzi wa rangi, kupatanisha na kulinda mazingira. Wakristo waliweza kujifunza kusikilizana na kushirikiana kikazi pamoja katika sehemu nyingi zenye tamaduni, desturi na penye imani mbalimbali au pasipo na imani yoyote. Bila hamasa ya 1910, sehemu kubwa ya ushirikiano huu isingewezekana.

## Kutafakari, Kuhakiki na Vitendo


Kwa miaka kadhaa iliyopita, pamekuwa na kikundi ambacho kinafanya kazi ya kuhakiki athari ya 1910 na kutafakari changamoto zinazoikabili misioni ya kikristo wakati huu. Ili kutimiza vizuri kazi hii,vikundi vingi vimekuwa vikishughulika na mada muhimu zinazohusika na asili na maana ya imani ya kikristo wakati huu. Vingine vimekuwa vikipanga jinsi sehemu nyingi, ikiwepo Edinburgh, zitakavyoweza kuienzi miaka hiyo mia moja ulimwenguni.

## Duniani na mahali ulipo

Mkutano wa 1910 ulifanyika katika mji asilia wa kimagharibi. Baada ya miaka mia moja, tunataka sherehe yetu iwe hakika ya ulimwengu mzima, pia mahali tulipo na kuhusisha wengi iwezekanavyo. Teknolojia ya kisasa na tovuti (Internet) zinatoa fursa ya kuwezesha jambo hili kutendeka. Mradi wetu wa 2010.global ni nafasi yako wewe ya kushirikiana na wengine sehemu ulipo, kumshukuru Mungu kwa pamoja juu ya karne hii ya misioni na kukabiliana na changamoto iliyopo mbele.

## Mchakato wa pande mbili

Mwaka 1910, mchakato ulitokea Edinburgh. Wakati huu, yaani 2010, sherehe na maoni yenu ulimwenguni yanatazamiwa kutoa ujumbe mpya kuelekea sasa Edinburgh. Patakuwa na tukio maalum litakalofanyika Edinburgh saa 14:00 GMT la kutafakari, kuonyesha shukrani kwa Mungu na kujitoa kwa moyo. Wakati huo huo, tunayahimiza makanisa na jamii za kikristo ulimwenguni kuandaa sherehe zao wenyewe. Kwa namna hii tunataka kuona jinsi kanisa ulimwenguni lilivyo na umoja na jinsi lilivyojizatiti kwa misioni ulimwenguni.







## 2010.global - Jinsi unavyoweza kuwa sehemu yake!

Jiunge na vikundi vya kikristo ulimwenguni unapoandaa sherehe za misioni Juni 2010 mahali ulipo. Inaweza kuwa wakati wowote mwakani kufuatana na jinsi unavyoona inawezekana kwenye mpango wako. Pia unaweza kuifanya Juni 6 ili kuunganika na wengine duniani. Unaweza kuifanya iwe

- Ibada ya pamoja na makanisa mengine
- Kuwa na mkesha wa vijana
- Kuwa na maigizo
- Kutembelea watu
- Sherehe za vikundi nyumbani

## Tumia kielekezo cha 2010.global kama mwongozo

Kama hujiamnini jinsi ya kuandaa sherehe- usijali, jaribu kwa kutumia kielekezo na maelezo zaidi kuhusu mradi katika tovuti **www.edinburgh2010.org**. Unaweza kutumia kielekezo hiki kuandaa sherehe yako kufuatana na jinsi unavyoona inafaa kufuatana na utamaduni wako. Tunatarajia kuona jinsi watu watakavyo sherehekea kutoka mahali walipo vijijini wakionyesha furaha yao, shukrani kwa Mungu na kujitoa kwa moyo ulimwenguni. Huu utakuwa ushuhuda mkuu kwa ajili ya upendo wa Mungu.

## Tengeneza ishara

Je unaweza kutengeneza ishara, alama au mchoro unaoonesha maana ya misioni ya Mungu kwako na kwa Wakristo katika sehemu ulipo duniani? Inaweza kuchukua ishara ya mlima mahali ulipo ambao hukukumbusha kuwepo kwa Mungu katika historia yako; au mizizi na matawi ya mti wa kiasili unaoleta maana ya ukuaji na upya wa maisha. Inaweza kuwa taswira kutoka kwenye bahari inayoonyesha kuwepo kwa roho ya Mungu katika jamii zetu. Mifano ni mingi sana! Unaweza kuiandaa pamoja katika kikundi, ukitumia msanii au kuandaa mashindano katika kanisa au shule ya jumapili. Unaweza pia kutengeneza beji, bendera, T-shirt au bango. Inaweza kuwa nembo au ishara ya kanisa lako. Itakuwa vizuri kama utaiweka kwenye tuvuti letu **www.edinburgh2010.org**, ili tuweze kuwa na maktaba ya picha zenu kutoka pote duniani.

## Omba pamoja nasi

Edinburgh 2010 inatoa Sala hii kwa matumizi ya wote ulimwengu na kama itikio la pamoja la shukrani kwa Mungu. Tafadhali andika na tushirikishe Sala ya eneo lako ili wengine waitumie.

*Mungu wa neema*
*Upendo wako unabubujika kwa wingi duniani*
*Umekuja karibu nasi na unagusa maumivu yetu,*
*Umewasha mioyo yetu kuwa na matumaini*
*Tunakurudishia shukrani,*
*Tunasherehekea misioni yako*
*Ya kupatanisha, kuponya na kutengeneza.*
*Tujaze Roho yako isiyozuilika ya upendo*
*Inayodhihirika kwetu katika jina la Kristo Yesu Bwana wetu.*
*Amen*





## Jiunge na tamasha kubwa ulimwenguni tarehe 6 Juni 2010

Tamasha ya misioni kule Edinburgh itafanyika Jumapili tarehe 6 Juni 2010, saa 14:00 GMT. Kwa nini usiwe na tamasha lako wakati huo huo? Kwa wale wa mashariki ina maana ya tamasha kufanyika usiku au wale wa magharibi itakuwa asubuhi. Wengine wataona haiwezekani na kuifanya wakati mwingine au siku nyingine muafaka. Inaweza kuwa tukio fulani la pekee au sehemu ya mpango mzima wa mahali ulipo. Edinburgh 2010 inatafiti uwezekano wa jinsi vikundi kwa njia ya tovuti vinaweza kuunganishwa na tukio la Edinburgh  Juni 6. Unakaribishwa kuona tovuti yetu **www.edinburgh2010.org** ili upate maelezo zaidi.

## Badili karamu iwe kitendo

- ➜ Jaribu kupanga kwa namna ambayo unajiwekea malengo ya tamasha lako kuwezeha kufuatilia momboa baada ya tamasha kama hatua zijazo katika Misioni ya Mungu katika mkoa wako. Itakuwa na msisitizo gani?
- ➜ Unaweza kukubaliana kuhusu mambo vya kufanya?
- ➜ Unaweza kumegeana na wengine duniani kuhusu mambo utakayofanya baada ya kutafakari na kumshukuru Mungu?
- ➜ Utawekaji haya katika mpango?
- ➜ Ni kitu gani utafanya tofauti wakati mambo yanabadilika duniani?
- ➜ Unaweza kufanya nini kwa kushirikiana na wakristo wengine badala ya kutenda peke yako?



## Tumia tovuti la Edinburgh 2010

Onyesha maono yako, ndoto na mpango kazi katika tovuti **www.edinburgh2010.org**, ili wengine waone na kuhamasishwa na uyafanyayo. Ukipanga tukio lolote kati ya Juni 6 au wakati mwingine, utaweza kupata maoni kutoka popote ulimwenguni yatakayokusaidia kuboresha dhamira yako hapo ulipo na mawazo yako yanaweza kuwasaidia wengine.

Kutokana na hayo, urafiki, ushirikiano na vikundi vinavyomegeana vitatokea. Mungu anaweza kutustaajabisha kwa njia hii.

## Kuwa Kijani

Uumbaji wa Mungu upo hatarini na wote tunawajibika kupunguza uchafuzi wa mazingira. Angalia tovuti yetu **www.edinburgh2010.org** kujua jinsi mipango *2010.global* inaweza kuwa ya kijani.

## Na Mwisho

Edinburgh 2010 itafanikiwa kama wote tutawajibika na kufanya kazi tuliyoitiwa na Mungu kuwa mawakili wa upendo, kuleta tumaini na uponyaji kwa watu wa Mungu ulimwenguni.







## Mashirika haya yanafadhili Edinburgh 2010

African Independent Churches, Anglican Communion, Asian Pentecostal Society, Baptist World Alliance, Church of Scotland, Churches Together in Britain and Ireland, Council for World Mission, International Association for Mission Studies, International Fellowship of Evangelical Students, Latin American Theological Fellowship, Lausanne Committee for World Evangelisation, Lutheran World Federation, Orthodox Churches, Roman Catholic Church, Seventh Day Adventist Church, World Alliance of Reformed Churches, World Council of Churches, World Evangelical Alliance, World Methodist Council, World Student Christian Federation

## Anwani

**Edinburgh 2010**
**Jasmin Adam**
**Communications Officer**
**email: jadam@cofscotland.org.uk**
**web: www.edinburgh2010.org**
Unaweza pia kutupata katika skype, facebook na twitter.

